WILAYA YA NYERI

DARASA LA TANO MWISHO WA MUHULA WA PILI - 2011

KISWAHILI : LUGHA

MUDA:
Saa. 1 Dakika 40

JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU
1. *Tumia penseli ya kawaida tu.*
2. *Hakikisha umeandika kwa karatasi ya majibu:-*
   (I) JINA LAKO *(II) JINA LA SHULE YAKO*

Jaza nafasi 1 -15 kwa majibu sahihi

Mtoto __1__ aliacha mchezo __2__ aliokuwa __3__ na akafuata maneno __4__ __5__ na __6__ maneno __7__ na baba __8__ . Na akatokea __9__ mtoto __10__ __11__ wote __12__ darasani __13__ . Kwa hivyo mtihani __14__ yeye ndiye __15__ kwa kwanza

1.	A. ule	B. yule	C. wale	D. vile
2.	A. yake	B. zake	C. wake	D. lake
3.	A. anayo	B . nalo	C. nako	D. nao
4.	A. aliyokuwa	B. aliokuwa	C. alizokuwa	D. alilokuwa
5.	A. akiifuata	B. akizifuata	C. akiyafuata	D. akiufuata
6.	A. akasingatia	B. akashikia	C. akaiyafuata	D. akizingatia
7.	A. aliambiwa	B. alipoambiwa	C. alizoambiwa	D. aliyoambiwa
8.	A. yake	B. wake	C. ake	D. wako
9.	A. kuwa	B. kua	C. kukua	D. kukuwa
10.	A. mhodari	B. hodari	C. mbora	D. mshujaa
11.	A. kumliko	B. kuwaliko	C. kuliko	D. kukiliko
12.	A. huo	B. hilo	C. hiyo	D. humo
13.	A. mwao	B. lao	C. yao	D. nao
14.	A. ulikuja	B. ulipokuja	C. uliyekuja	D. ikipokuja
15.	A. akikuwa	B. akakua	C. akawa	D. akuwe

Kutoka swali la 16 - 30 jibu kulingana na maagizo

16. Andika tarakimu hii kwa maneno: 100,000
   A. Mia kumi B. Laki mia moja
   C. Laki moja D. Elfu kumi
17. Chakula cha asubuhi hujulikana kama _____
   A. chajio B. kishuka C. kitoweo D. staftahi
18. Kamilisha methali hii
   Mungu si _____
   A. muunguana B. mjinga
   C. athumani D. mnono
19. Kinyume cha **mnene** ni?
   A. mkonde B. mwembamba
   C. mrefu D. mpole
20. Kamilisha sentensi.
   Kiroboto _____ huwa na matatizo mengi
   A. hiki B. huyu C. hii D. huu
21. Nilimuua simba _____ paka
   A. ila B. sembuse C. wala D. pia
22. Wakati wa baridi kali huitwa
   A. Masika B. Kiangazi
   C. Kipupwe D. Kusi
23. Wakati wa usiku watu huagana vipi?
   A. Hujambo B. Usiku
   C. Lala D. Alamsiki
24. Dada ya baba yako hutamwita?
   A. Mjomba B. Halati
   C. Shangazi D. Wifi
25. Hili umbo linaitwaje?



   A. Pia
   B. Mche
   C. Mstatilili
   D. Kopa
26. Andika sudusi mbili kwa tarakimu
   A. $^2/_3$ B. $^2/_7$ C. $^2/_6$ D. $^2/_5$
27. Sijamuona Musa _____ jana
   A. toka B. mpaka
   C. tangu D. mpaka wa
28. Chakula kilicholala huitwa?
   A. kiporo B. kishuka
   C. mabaki D. masalia
29. Neno jingine lenye maana sawa na ***runinga*** ni
   A. redio B. ngoma
   C. televisheni D. kinanda
30. Kitanda hiki ni cha _____ mtoto mchanga.
   A. kumlalisha B. kumlazia
   C. kumlalia D. kumlashia

Soma shairi hili kisha ujibu maswali 31 -40

Naanza yangu ***Kauli,*** nina yangu matamko
Kuwaambia ukweli, kwa hiki changu ***kimako***
Tangu jadi na asili, ni jambo limekuwako
Watu wema wapi, wasiokuwa na wivu

Ni wachache hao wema, wasiopenda ***vituko***
Wapingao dhuluma, ubaya kwao ni mwiko
Wasotaka uhasama, kupinga michafuko
Watu wema wako wapi, wasiokuwa na wivu

Nimefika ***ukingoni,*** yameisha ***matamko***
Kwenda mbele sitamani, ninarudi nitokako
Nitafanya juu chini, ***kusaka*** wema waliko
Watu wema wako wapi, wasiokuwa na wivu

31. Shairi hili lina beti ngapi?
A. 3 B. 4 C. 5 D. 6
32. Neno ***ukingoni*** limaanisha
A. katikati B. tayari C. mwisho D. mwanzo
33. Mistari ya shairi hujulikana kama
A. beti B. kibwagizo C. mishororo D. vituo
34. Kinyume cha ***wema*** ni
A. ukingoni B. uhasama
C. utovu D. ubaya
35. Maana ya neno ***Kusaka*** ni _____
A. kutafuta B. kujibu C. kuuliza D. vituko
36. Fungu la mishororo katika shairi huitwa
A. kina B. ubeti
C. mshororo D. kibwagizo
37. Katika ubeti wa mwisho mwandishi anasema arudi wapi?
A. Kwao B. Kusaka
C. Kutafuta watu wema D. Hatujaelezwa
38. Nyimbo huimbwa, Je shairi ___
A. husomwa B. hukaririwa
C. huimbwa pia D. hukogwa
39. Tangu jadi na asili maana ya maneno haya kama yalivyotumika ni _____
A. tangu zamani za kale
B. tangu utotoni
C. tangu uhasama kuanza
D. tangu waanze matamko
40. Kicha mwafaka cha shairi hili ni
A. kimako B. wivu mbaya
C. shairi kavu D. uhasama

Soma habari ifuatayo na ujibu maswali 41 -50

Serikali yetu haiwashughulikii watu wanaojiweza pekee. Huwashughulikia walemavu pia. Ulemavu husababishwa na sehemu yoyote ya mwili kutofanya kazi ya kawaida.

Walemavu ni watu kama wasioona, viguru au viwete. Walemavu hupelekwa shule maalum. k.m kuna shule za kuwafunzia vipofu, walioharibika miguu, walio na shida za akili na wasiosikia.

Katika shule hizi, walemavu hufunzwa jinsi ya kujitunza badala ya kuwategemea watu wengine

41. Serikali huwashughulikia
A. watu wasiojiweza B. watu wote
C. watu wanaojiweza D. viwete
42. Ulemavu ni
A. ungonjwa
B. sehemu yoyote kutofanya kazi
C. kushindwa kufanya kazi
D. kutofanya kazi yoyote
43. Wasioona, wasiosikia na viwete huitwa
A. vipofu B. viguru
C. walemavu D. vilema
44. Ulemavu aina ngapi umetanjwa katika habari hii?
A. Tano B. Sita C. Tatu D. Nne
45. Walemavu hupelekwa shule gani?
A. Za kawaida B. Za upili
C. Maalum D. Za serikali
46. Katika shule walemavu hufunzwa
A. Kujitunza
B. Kutegemea na wenzao
C. Kupigana na wasio walemavu
D. Sehemu za mwili
47. Ukiwa na mtoto aliyelemaa, yafaa _____
A. umchukie
B. umfiche nyumbani
C. umtunze nyumbani
D. umpeleke katika shule maalum
48. Kwa mujibu wa taarifa uliyoisoma walemavu wasiposoma
A. Hawataweza kufanya kazi za kawaida
B. Hawatajitegemea
C. Hawatajiunga na shule maalum
D. Serikali haitajenga shule maalum
49. Ni methali gani imetaja walemavu katika hizi?
A. Mcheka kilema hafi hakijamfika
B. Mwamuzi chake ni kigongo
C. Mpanda farasi wawili hupasuka msamba
D. Mgeni pofu ingawa ana macho yake
50. Kichwa kinachofaa habari hii ni
A. Huduma za serikali
B. Kujitegemea
C. Walemavu
D. Walioharika